**BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**

70 Barabara ya Chukwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI (PAC) KUHUSU UWASILISHWAJI WA RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2023

**Mheshimiwa Spika,** naanza kumshukuru Mwenyezi Mungu, Bwana wa viumbe vyote, Muumba Mbingu na Ardhi pamoja na vilivyomo ndani yake, ambae ametujaalia uhai, afya njema na taufiki ya kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa lengo la kutekeleza majukumu yetu ya kuwatumikia wananchi wa Zaznzibar.

**Mheshimiwa Spika** pia nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika kwa kunipa nafasi hii ya kusimama mbele ya Baraza lako Tukufu ili niweze kuzungumzia machache na ya muhimu, yanayohusu uwasilishwaji wa Ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi cha mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023 kama ambavyo Kanuni ya 43(1) ya kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la mwaka 2020 inavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kumshukuru Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa kuweza kuwasilisha hapa Barazani Ripoti hizi ambazo ndio zinazotumiwa na Kamati yetu ya kuchunguza Mapato na Matumizi ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, napenda kutoa pongezi na shukurani za dhati kwa Wajumbe na Makatibu wa Kamati hii kwa umahiri wao na umakini mkubwa walionao wakati wote wa utekelezaji wa kazi za Kamati ikiwa ni pamoja na kazi hii ya kuzipitia na kuzichambua Ripoti zote za Ukaguzi zilizowasilishwa hapa Barazani.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wao, naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. Mhe. Juma Ali Khatib | - | Mwenyekiti; |
| 2. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa | - | M/Mwenyekiti; |
| 3. Mhe. Bakar Hamad Bakar | - | Mjumbe; |
| 4. Mhe. Miraji Khamis Mussa | - | Mjumbe; |
| 5. Mhe. Mohamed Ahmada Salum | - | Mjumbe; |
| 6. Mhe. Kombo Mwinyi Shehe | - | Mjumbe; |
| 7. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman | - | Mjumbe; |
| 8. Mhe. Jamal Kassim Ali | - | Mjumbe; |
| 9. Ndg. Fatma Omar Ali | - | Katibu; |
| 10. Ndg. Maryam Haji Ali | - | Katibu; |
| 11. Ndg. Said Khamis Ramadhan | - | Katibu; na |
| 12. Ndg. Adam Maulid Simai | - | Katibu. |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya PAC inatambua, kuheshimu na kuthamini kazi kubwa inayofanywa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, katika kujenga nidhamu ya ukusanyaji wa Mapato na Matumizi ya Rasimali za Umma katika Serikali na kuimarisha misingi ya Demokrasia na Utawala Bora hapa nchini hasa ikizingatiwa kuwa Sheria za Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Namba 11 ya mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Namba 12 ya mwaka 2016 zinaelekeza utaratibu na nidhamu ya Matumizi yanayofanywa na Wizara na Taasisi za Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mnasaba huo, Kamati yangu ina kila sababu ya kuwapongeza kwa dhati Viongozi na Watendaji wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa utekelezaji wa kazi ngumu ya udhibiti na ukaguzi na hatimae kumudu kuandaa Ripoti hizi kama ambavyo kifungu cha 112 cha Katiba yetu kinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** kwa vile udhibiti na ukaguzi ni dhana pana inayohitaji kutekelezwa kwa utaalamu na uweledi wa hali ya juu, hivyo, Afisi ya Baraza la Wawakilishi inaiomba Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali iendelee kuipatia mafunzo ya mara kwa mara Kamati hii inayosimamia masuala ya Kifedha yakiwemo mafunzo ya utambuzi wa mbinu mpya na aina mbali mbali za Ukaguzi na Udhibiti ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati hii.

**Mheshimiwa Spika,** jumla ya Ripoti nane zilizowasilishwa hapa Barazani ambazo Kamati yetu inatarajia kuzifanyia kazi mara tu baada ya kukabidhiwa na Mheshimiwa Spika wa Baraza letu hili. Ripoti hizo zinahusiana na:

1. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;
2. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;
3. Ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;
4. Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Tawala za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;
5. Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma na Taasisi zinazojitegemea za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;
6. Ukaguzi wa Kiufundi wa Ukarabati wa Uwanja wa Michezo Gombani Chake Chake Pemba kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;
7. Ukaguzi wa Kiufundi wa Ujenzi wa Hospitali Kumi za Wilaya na Hospitali Moja ya Mkoa kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023; na
8. Ukaguzi wa Kiufundi wa Mradi wa Usambazaji wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama Unguja na Pemba kwa kipindi cha mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2023;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali imezipokea Ripoti zote hizo na kuahidi kuzifanyia kazi na kuwasilisha kwa kina taarifa zake mbele ya Baraza hili Tukufu ili Waheshimiwa Wajumbe mupate nafasi ya kuichangia, kutoa Maoni, Mapendekezo na hatimae Serikali kuchukua hatua stahiki kwa Watendaji wote waliohusika na ubadhirifu na upotevu wa fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** mambo ya jumla ambayo Kamati imeyabaini kupitia

Ripoti zilizowasilishwa ni:

## (A) UWASILISHWAJI WA RIPOTI ZA UKAGUZI WA KIUFUNDI

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya PAC imepokea Ripoti za Ukaguzi wa kiufundi zilizowasilishwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusiana na Ukaguzi wa Ujenzi wa Hospitali Kumi za Wilaya na Hospitali Moja ya Mkoa, Mradi wa Usambazaji wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama

kwa Unguja na Pemba na Ukarabati wa Uwanja wa Michezo Gombani Chake Chake Pemba.

**Mheshimiwa Spika,** ni matumaini ya Kamati yetu kwamba kuwasilishwa kwa ripoti hizi za kiufundi mbele ya Baraza lako Tukufu zitaenda kuleta mageuzi makubwa katika usimamizi madhubuti wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayoendelea kutekelezwa na Serikali yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kiujumla, Ripoti hizo zimebainisha uwepo wa dosari kadhaa zilizojitokeza zinazoashiria uwepo wa uwezekano wa ubadhirifu na upotevu wa mabilioni ya fedha za Serikali uliotokana na usimamizi na utekelezaji usioridhisha wa Miradi hiyo. Kwa mfano katika Sekta ya Afya, kuna jumla ya bilioni 18,521,528,457 zimeelezwa kuongezeka katika Ujenzi wa Hospitali Kumi za Wilaya ambapo hali hii imetokana na kushindwa kwa wataalamu kuandaa vyema Tathamini ya Mahitaji na kupelekea kuwepo kwa ongezeko kubwa za fedha ambazo zipo kinyume na makubaliano ya mkataba wa awali.

**Mheshimiwa Spika,** licha ya Serikali kutenga Bajeti ya shilingi bilioni 7,000,000,000 kila mwaka kwa ajili ya kuendeleza Ujenzi wa Viwanja vya Michezo Zanzibar. Hata hivyo, Kamati yetu imepitia Ripoti husika ambayo imeeleza kuwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo imetekeleza ukarabati wa Mradi wa Uwanja wa Michezo wa Gombani Pemba ukiwa na dosari lukuki ambazo kwa kiasi kikubwa zinatia wasiwasi juu ya gharama zilizotumika pamoja na utaratibu uliotumika katika ukamilishaji wa Mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** Ripoti imeeleza wazi kwamba katika utekelezaji wa Mradi huo, Wizara ilitumia jumla ya shilingi bilioni 5.642 ambapo shilingi bilioni 2.8 zilitumika katika awamu ya mwanzo ya ukarabati na kukawa na ongezeko la shilingi bilioni 2.842 ikiwa ni gharama zilizoainishwa katika nyongeza ya Mkataba wa awali. Kwa msingi huo, Kamati yetu imepanga kuzifuatilia kwa karibu kasoro zilizoibuliwa katika Ripoti husika ili kubaini taswira halisi ya uwepo wa ongezeko lililojitokeza.

**Mheshimiwa Spika,** wakati Kamati yetu ikipitia Ripoti ya Kiufundi ya Usambazaji wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama, imebainika kuwa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) ilitakiwa kusimamia ipasavyo utekelezaji wa Mradi huo. Hata hivyo, kumejitokeza kasoro kadhaa katika ujenzi wa vituo vya usambazaji maji zilizoainishwa katika Ripoti ya Mdhibiti zikiwemo kujengwa kwa visima vyenye kina cha mita 17 mpaka 98 lakini hakukuwa na kisima kilichojengwa kufikia kina cha mita 150 kama ilivyohitajika kwenye Mkataba.

Zaidi ya hilo, malipo yalifanywa kwa gharama za uchimbaji wa visima vyenye kina cha mita 150 na kupelekea kuwepo kwa hasara ya shilingi bilioni 928,153,089.48.

**Mheshimiwa Spika,** sambamba na hayo, visima vyenye jumla ya kina cha mita 3,309.49 ambazo zilihitajika kuchimbwa hazikuweza kuchimbwa lakini malipo yalifanyika kinyume na masharti ya Mkataba. Aidha, Kamati yetu imebaini kuwepo kwa mabadiliko ya malipo ya viwango vya Mkandarasi kwa daraja halisi la C40 katika ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji ambayo yamepelekea kuongeza gharama za Mradi kwa shilingi bilioni 1,474,240,021.75 ikijumuisha VAT. Mheshimiwa Spika, Ripoti imebaini kuwa kuchelewa kukamilika kwa miradi hiyo kumepelekea ongezeko la shilingi bilioni 202,705,283.33 katika ujenzi wa matangi ya maji.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati yetu inaahidi kuzichunguza kwa undani dosari zote zilizobainika na kuwasilisha ripoti yake mbele ya Baraza hili ambayo itaweza kubainisha kama kweli kuna upotevu na ubadhirifu wa fedha za umma ama vyenginevyo kwa kutumia njia tofauti za kiuchunguzi.

**(B) KUJIRUDIA KWA DOSARI KADHAA AMBAZO ZILIBAINIKA KATIKA UKAGUZI ULIOPITA WA MWAKA 2021/2022**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali inasikitishwa na kushangazwa kwamba pamoja na kubainika dosari kupitia ukaguzi uliopita na juhudi kadhaa kuchukuliwa ili kurekebishwa kwa kasoro hizo. Hata hivyo, bado kuna Taasisi zinaonekana hazioneshi mabadiliko ya matokeo chanya kwani dosari ambazo zimeripotiwa katika Ripoti zilizopita, zimeendelea kujitokeza tena katika Ripoti za Mwaka huu. Kamati imebaini hayo baada ya kupitia Ripoti hizo za Ukaguzi zilizowasilishwa ambapo dosari zifuatazo zimebainika kujirudia, miongoni mwa dosari hizo ni:

1. Kutokuthibitishwa kazini kwa waajiriwa waliomaliza muda wa majaribio (Probation period);
2. kutokujumuishwa kwa fedha za Matumizi katika Taarifa ya Hesabu za Mwisho wa mwaka;
3. Malipo kwa watoa huduma ambao hawakusajiliwa na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma;
4. Malipo ambayo hayakukatwa kodi ya zuio;
5. Matumizi yaliyofanyika nje ya bajeti;
6. Kukosekana kwa Mapato yatokanayo na ukodishwaji wa majengo;
7. Fedha zilizolipwa kwa njia taslim;
8. Kutowasilishwa kwa Mapato katika Mfuko Mkuu wa Hazina;

9. Kuwepo kwa malimbikizo ya madeni tofauti; na
10. Kukosekana kwa Mikataba ya utoaji wa huduma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa msingi huo, Kamati ya PAC itazifanyia kazi ipasavyo Ripoti hizi na hatimae kuwasilisha Ripoti yake kwa kina hapa Barazani katika muda muafaka, kama Kanuni za Kudumu za Baraza hili zinavyoelekeza.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia naomba kuishukuru Afisi ya Baraza la Wawakilishi kwa ushirikiano mkubwa inayoipatia Kamati yetu wakati wa kutekeleza majukumu yake ikiwemo utekelezaji wa kazi hii ya kuchambua na kutoa Maoni ya Kamati juu ya uwasilishwaji wa Ripoti hii ya Ukaguzi. Nawashukuru pia Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, kwa kunisikiliza kwa umakini na kwa utulivu mkubwa wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuwasilisha.

……………………
Mhe. Juma Ali Khatib,
Mwenyekiti,
Kamati ya Kudumu ya Kuchunguza na Kudhibiti
Hesabu za Serikali (PAC),
**BARAZA LA WAWAKILISHI,**
**ZANZIBAR.**